



1-IMANI

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allaah Ar-Rahmaan, Mwenye kurehemu.

Namuomba Allaah Mkarimu, Rabb wa ‘Arshi Adhimu, Akuhifadhi duniani na Aakhirah, na Akujaalie mwenye baraka popote ulipo, na Akujaalie miongoni mwa wale; anapopewa hushukuru, na anapotaribiwa mitihani husubiri, na anapotenda dhambi huomba maghfirah, kwani mambo hayo matatu ni funguo za furaha.

Fahamu, Akuongoze Allaah katika utiifu Wake, kwamba Haniyfiyyah (Kuelemea katika Dini ya haki na kujiepusha na dini potofu) ni Dini ya Ibraahiym, umwabudu Allaah Pekee, ukiwa ni mwenye kumtakasia Dini Yake.

kama Anavyosema Ta'aalaa:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ (٥٦)

((Na Sikuumba majini na wanadamu isipokuwa waniabudu))[2]

Basi utakapojua kwamba Allaah Amekuumba kwa ajili ya kumwabudu Yeye, basi jua kwamba: 'Ibaadah haiitwi 'ibaadah isipokuwa pamoja na Tawhiyd (kumpwekesha Allaah), kama ambavyo Swalaah haiitwi Swalaah isipokuwa pamoja na twahaarah.

Hivyo basi itakapoingia shirki katika 'ibaadah inaharibika kama najsi inavyoingia katika twaaharah (inaitengua).

Na utakapojua kwamba shirki inapochanganyika na 'ibaadah inaiharibu na inaporomosha 'amali, na mtendaji huwa ni miongoni mwa watakaodumu motoni, hapo utajua kwamba jambo muhimu kabisa kwako (la kuwajibika) ni utambuzi wa hilo, huenda Allaah Akuepushe katika utando wa utata huu.

Navyo ni kumshirikisha Allaah ambayo Allaah Ta'aalaa Anasema:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ ۚ وَمَنْ يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ افْتَرَىٰ إِثْمًا عَظِيمًا (٤٨)

((Hakika Allaah Haghufuri kushirikishwa; lakini Anaghufuria yasiyokuwa hayo kwa Amtakae))[3]

Kwa Jina la Allaah Ar-Rahmaan, Mwenye kurehemu.

Fahamu, Allaah Akurehemu, kwamba ni wajibu wetu kujua mas-alah manne:

Suala la kwanza: Elimu:

Nayo ni elimu ya kumjua Allaah, na elimu ya kumjua Nabi Wake (صلى الله عليه وآله وسلم) na elimu ya kuijua Dini ya Kiislamu kwa dalili.

Suala la pili: Kuifanyia kazi.

Suala la tatu: Kuilingania.

Suala la nne: Kuwa na subira katika maudhi yatakayopatikana ndani yake.

Na dalili ni kauli Yake Ta'aalaa:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ
وَالْعَصْرِ (١) إِنَّ الْإِنْسَانَ لَفِي خُسْرٍ (٢) إِلَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا
الصَّالِحَاتِ وَتَوَاصَوْا بِالْحَقِّ وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ (٣)

Kwa Jina la Allaah, Ar-Rahmaan, Mwenye kurehemu.

((Naapa kwa Al-‘Aswr (zama). Hakika mwana wa Aadam bila shaka yumo katika khasara. Isipokuwa wale walioamini na wakatenda mema na wakausiana haki na wakausiana subira)) [2]

Na dalili ni kauli Yake Ta’aalaa:

فَاعْلَمْ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاسْتَغْفِرْ لِذَنْبِكَ

((Basi jua kwamba laa ilaaha illa-Allaah, hapana muabudiwa wa haki ila Allaah na omba maghfirah kwa dhambi zako.))[3]

Akaanza kwa elimu kwanza kabla ya kauli na ‘amali.

Fahamu Allaah Akurehemu, kwamba ni wajibu kwa kila Muislamu mwanamme na Muislamu mwanamke, kujifunza mas-alah haya matatu na kuyafanyia kazi:

La kwanza: Kwamba Allaah Ametuumba, na Anaturuzuku, na Hakutuacha bure bali Ametutumia Rasuli. Basi atakayemtii ataingia Jannah, na atakayemuasi ataingia motoni.

Na dalili ni kauli Yake Ta’aalaa:

إِنَّا أَرْسَلْنَا إِلَيْكُمْ رَسُولًا شَاهِدًا عَلَيْكُمْ كَمَا أَرْسَلْنَا إِلَىٰ فِرْعَوْنَ رَسُولًا (١٥) فَعَصَىٰ فِرْعَوْنُ الرَّسُولَ فَأَخَذْنَاهُ أَخْذًا وَبِيلًا (١٦)

((Hakika Sisi Tumekutumieni Rasuli awe shahidi juu yenu, kama Tulivyotuma Rasuli kwa Fir’awn. Lakini Fir’awn alimuasi huyo Rasuli, Tukamshika kwa maangamizi makali mno))[4]

La pili: Kwamba Allaah Haridhii kushirikishwa pamoja Naye yeyote yule katika ‘ibaadah Yake, ikiwa ni Malaika aliyekurubishwa, wala Nabiyy aliyetumwa kuwa Rasuli.

Na dalili ni kauli Yake Ta’aalaa:

وَأَنَّ الْمَسَاجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدْعُوا مَعَ اللَّهِ أَحَدًا (١٨)

((Na kwamba Misikiti ni kwa ajili ya Allaah, basi msiombe yeyote pamoja na Allaah))[5]

La Tatu: Kwamba Atakayemtii Rasuli, na Akampwekesha Allaah, haijuzu kwake kufanya urafiki na ushirikiano na yule anayempinga Allaah na Rasuli Wake hata akiwa ni jamaa wa karibu.

Na dalili ni kauli Yake Ta’aalaa:

لَا تَجِدُ قَوْمًا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ يُوَادُّونَ مَنْ حَادَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَوْ كَانُوا آبَاءَهُمْ أَوْ أَبْنَاءَهُمْ أَوْ إِخْوَانَهُمْ أَوْ عَشِيرَتَهُمْ أُولَئِكَ كَتَبَ فِي قُلُوبِهِمُ الْإِيمَانَ وَأَيَّدَهُم بِرُوحٍ مِّنْهُ وَيُدْخِلُهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ أُولَئِكَ حِزْبُ اللَّهِ أَلَا إِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْمُفْلِحُونَ (٢٢)

((Hutokuta watu wanaomuamini Allaah na Siku ya Mwisho kuwa wanafanya urafiki na kuwapenda ambaye anapinzana na Allaah na Rasuli Wake, japo wakiwa ni baba zao, au watoto wao, au ndugu zao, au jamaa zao. Hao (Allaah) Amewaandikia katika nyoyo zao iymaan, na Akawatia nguvu kwa Ruwh (Wahyi) kutoka Kwake, na Atawaingiza Jannaat zipitazo chini yake mito ni wenye kudumu humo. Allaah Ameridhika nao, nao wameridhika Naye. Hao ndio

kundi la Allaah. Tanabahi! Hakika kundi la Allaah ndio lenye kufaulu))[6]

Fahamu, Allaah Akuongoze katika utiifu Wake, kwamba *al-Hanifiyyah* (kuelemea Dini ya haki na kujiepusha na dini potofu) ni Dini ya Ibraahiym. Umwabudu Allaah Pekee ukimtakasia Dini Yake, na kwa hilo Allaah Amewaamrisha watu wote, na Amewaumba kwa sababu hiyo.

Kama Anavyosema Ta’aalaa:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ (٥٦)

((Na Sikuumba majini na wanadamu isipokuwa waniabudu))[7]

Na maana ya ((waniabudu)) ni: Wanipwekeshe. Na jambo kuu kabisa Aloamrisha Allaah ni At-Tawhiyd ambayo ni: Kumpwekesha Allaah katika ‘ibaadah. Na jambo kuu kabisa Alokataza ni shirki, ambayo ni: kumuomba mwengine pamoja Naye.

Na dalili ni kauli Yake Ta’aalaa:

وَاعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا

((Na mwabuduni Allaah na wala msimshirikishe na chochote))[8]

Basi utakapoulizwa: “Nini Al-Uswuwul ath-Thalaathah (misingi mitatu) ambayo mwana wa Adam anawajibika kuifahamu?”

Sema: “Mja kumjua Rabb wake, na Dini yake, na Nabiyy wake (صلى الله عليه وآله وسلم) Muhammad

Msingi Wa Kwanza: Kumjua Rabb:

Basi utakapoulizwa: “Nani Rabb wako?”

Sema: “Rabb wangu ni Allaah Aliyenilea na Aliyewalea walimwengu wote kwa neema Zake. Naye Ndiye Ninayemwabudu, na sina mwengine ninayemwabudu.

Na dalili ni kauli Yake Ta’aalaa:

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ (٢)

((AlhamduliLLaah Himidi Anastahiki Allaah Rabb wa walimwengu))[9]

Na kila kitu kisichokuwa Allaah, ni kilichoumbwa nami ni mmojawapo katika kilichoumbwa.

Basi utakapoulizwa: “Umemjuaje Rabb wako?”

Sema: “Kutokana na Aayaat (ishara) Zake na Alivyoviumba. Na miongoni mwa Aayaat Zake ni: Usiku, mchana, jua, mwezi. Na miongoni mwa Alivyoviumba ni mbingu saba na ardhi saba, na kila kilichokuwemo ndani yake na baina yake”

Na dalili ni kauli Yake Ta’aalaa:

وَمِنْ آيَاتِهِ اللَّيْلُ وَالنَّهَارُ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ ۚ لَا تَسْجُدُوا لِلشَّمْسِ وَلَا لِلْقَمَرِ وَاسْجُدُوا لِلَّهِ الَّذِي خَلَقَهُنَّ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ (٣٧)

((Na katika Aayaat (ishara, dalili) Zake, ni usiku na mchana, na jua na mwezi. Msisujudie jua wala mwezi; bali msujudieni Allaah Ambaye Aliyeviumba ikiwa Yeye Pekee mnawambudu))[10]

Na kauli Yake Ta’aalaa:

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ يُغْشِي اللَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهِ ۗ أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ (٥٤)

((Hakika Rabb wenu ni Allaah Ambaye Ameumba mbingu na ardhi katika siku sita, kisha Istawaa juu ya ‘Arshi;[11] Anafunika usiku kwa mchana, unaufuatia upesi upesi na (Ameumba) jua na mwezi na nyota (vyote) vimetiishwa kwa amri Yake. Tanabahi! Ni Vyake Pekee uumbaji na amri. Tabaaraka Allaah, Amebarikika Allaah Rabb wa walimwengu))[12]

Na Rabb Ndiye Mwenye kuabudiwa

:Na dalili ni kauli Yake Ta’aalaa

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اعْبُدُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ وَالَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ (٢١) الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ فِرَاشًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً وَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجَ بِهِ مِنَ الثَّمَرَاتِ رِزْقًا لَكُمْ ۖ فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أَنْدَادًا وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ (٢٢)

((Enyi watu! Mwabuduni Rabb wenu Ambaye Amekuumbeni na wale wa kabla yenu mpate kuwa na taqwa. Ambaye Amewafanyieni ardhi kuwa ni tandiko na mbingu kuwa ni paa, na Akateremsha kutoka mbinguni maji, Akawatolea kwayo matunda kuwa ni riziki zenu. Basi msimfanyie Allaah waliolingana naye na hali ya kuwa nyinyi mnajua))[13]

Ibn Kathiyr (رحمه الله) amesema: “Muumbaji wa vitu hivi Ndiye Anayestahiki kuabudiwa. Na aina za ‘ibaadah ambazo Allaah Ameziamrisha ni mfano: *Al-Islaam* (Uislamu), *Al-Iymaan* (Imani),

Al-Ihsaan (Ihsani). Miongoni mwazo ni: *Ad-Du'aa* (du'aa), *Al-Khawf* (khofu ya kuogopa mtu au adhabu au kitu), *Ar-Rajaa* (kutarajai), *At-Tawakkul* (kutawakali kwa Allaah), *Ar-Raghbah* (shauku, utashi na matumaini ya jambo la kupendwa), *Ar-Rahbah* (tisho au kuogopa), *Al-Khushuu'* (unyenyekevu), *Al-Khashyah* (khofu kutokana na utukufu wa Allaah nayo inahusiana na elimu), *At-Taqwa* (uchaji), *Al-Inaabah* (kurejea kutubu na utiifu), *Al-Isti'aanah* (kuomba msaada wa mambo ya kidunia au ya Aakhirah), *Al-Isti'aadhah* (kuomba kinga), *Al-Istighaathah* (kuomba msaada, kuokolewa, au kufarijiwa jambo au haja wakati wa shida au kuokolewa), *Adh-Dhab-hu* (kuchinja), *An-Nadhru* (kuweka nadhiri), na mengineyo ya aina za 'ibaadah ambazo Allaah Ameziamrisha. Zote ziwe kwa ajili ya Allaah Ta'aalaa.

:

Na dalili ni kauli Yake:

وَأَنَّ الْمَسَاجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدْعُوا مَعَ اللَّهِ أَحَدًا (١٨)

((Na kwamba Misikiti ni kwa ajili ya Allaah, basi msiombe yeyote pamoja na Allaah))[14]

Basi atakayeelekeza chochote katika hizo ('ibaadah) kwa asiye kuwa Allaah, basi yeye ni mshirikina, kafiri.

Na dalili ni kauli Yake Ta'aalaa:

وَمَنْ يَدْعُ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ لَا بُرْهَانَ لَهُ بِهِ فَإِنَّمَا حِسَابُهُ عِنْدَ رَبِّهِ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الْكَافِرُونَ (١١٧)

((Na yeyote yule anayeomba du'aa (au kuabudu) pamoja na Allaah mungu mwengine hana ushahidi wa wazi wa hilo; basi hakika hesabu yake iko kwa Rabb wake. Hakika hawafaulu makafiri))[15]

وَفِي الْحَدِيثِ: ((الدُّعَاءُ مَخِ الْعِبَادَةِ))

Na katika Hadiyth: ((*Du'aa* ni ubongo wa 'Ibaadah))

[Hadiyth hii ni dhaifu. Ameipokea At-Tirmidhiy - Taz Al-Mishkaat (2331). Lakini ipo Hadiyth kama hiyo ambayo ni sahihi isemayo ((*Du'aa ni 'Ibaadah*)) Taz. Swahiyh Al-Jaami' Asw-Swaghiyr (3407)]

Na dalili ni kauli Yake Ta'aalaa:

وَقَالَ رَبُّكُمْ ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي
سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ (٦٠)

((Na Rabb wenu Amesema: “Niombeni, Nitakuitikieni. Hakika wale wanaotakabari katika kuniabudu wataingika Jahanam wadhalilike))
[16]

Na dalili ya *Al-Khawf* (kukhofu) ni kauli Yake Ta'aalaa:

فَلَا تَخَافُوهُمْ وَخَافُونَ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ (١٧٥)

((Basi msiwakhofu, na nikhofuni Mimi mkiwa ni Waumini))[17]

Na dalili ya *Ar-Rajaa* (kutaraji) ni kauli Yake Ta'aalaa:

فَمَنْ كَانَ يَرْجُو لِقَاءَ رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَالِحًا وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ
رَبِّهِ أَحَدًا (١١٠)

((Hivyo anayetaraji kukutana na Rabb wake, basi na atende ‘amali njema na wala asishirikishe yeyote katika ‘ibaadah za Rabb wake’))
[18]

Na dalili ya *At-Tawakkul* (kutawakali, kutegemea) kauli Yake Ta'aalaa:

وَعَلَى اللَّهِ فَتَوَكَّلُوا إِن كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ (٢٣)

((Na kwa Allaah Pekee tawakalini ikiwa nyinyi ni Waumini))[19]

Na kauli Yake:

وَمَنْ يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُ ج

((Na yeyote anayetawakali kwa Allaah, basi Yeye Humtosheleza))
[20]

Na dalili ya *Ar-Raghbah* (shauku, utashi na matumaini ya jambo la kupendwa) na *Ar-Rahbah* (tisho au kuogopa) na *Al-Khushuu'* (unyenyekevu) ni kauli Yake Ta'aalaa:

إِنَّهُمْ كَانُوا يُسَارِعُونَ فِي الْخَيْرَاتِ وَيَدْعُونَنَا رَغَبًا وَرَهَبًا وَكَانُوا لَنَا خَاشِعِينَ (٩٠)

((Hakika wao walikuwa wakikimbilia katika mambo ya kheri, na wakituomba kwa raghba na khofu, na walikuwa wenye kutunyenyekesha))[21]

Na dalili ya *Al-Khashyah* (khofu kutokana na utukufu wa Allaah nayo inahusiana na elimu), ni kauli Yake Ta'aalaa:

فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنِي

((Basi msiwaogope bali Niogopeni))[22]

Na dalili ya *Al-Inaabah* (kurejea kutubu na utiifu) ni kauli Yake:

وَأَنِيبُوا إِلَىٰ رَبِّكُمْ وَأَسْلِمُوا لَهُ

((Na rudini kila mara kutubu kwa Rabb wenu na jisalimisheni Kwake))[23]

Na dalili ya *Al-Isti'aanah* (kuomba msaada wa mambo ya kidunia au ya Aakhirah) ni kauli Yake Ta'aalaa:

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ (٥)

((Wewe Pekee tunakuabudu na Wewe Pekee tunakuomba msaada))
[24]

وَفِي الْحَدِيثِ: ((...وَإِذَا اسْتَعْنَتْ فَاسْتَعْنِ بِاللَّهِ))

Na katika Hadiyth: ((Ukitaka kuomba msaada, basi mwombe Allaah))[25]

Na dalili ya *Al-Isti'aadhah* (kuomba kinga) ni kauli Yake Ta'aalaa:

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ (١) وَ قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ (١)

((Sema: “Najikinga na Rabb wa mapambazuko”))[26]na ((Sema: “Najikinga na Rabb wa watu”))[27]

Na dalili ya *Al-Istighaathah* (kuomba msaada, kuokolewa, au kufarijiwa jambo au haja wakati wa shida au kuokolewa), ni kauli Yake Ta'aalaa:

إِذْ تَسْتَغِيثُونَ رَبَّكُمْ فَاسْتَجَبْ لَكُمْ

((Na (kumbukeni) pale mlipomuomba ukovu Rabb wenu Naye Akakuitikieni))[28]

Na dalili ya *Adh-Dhab-h* (kuchinja) kauli Yake Ta'aalaa:

قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ
(١٦٢) لَا شَرِيكَ لَهُ ۚ وَبِذَلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ (١٦٣)

((Sema: “Hakika Swalaah yangu, na kuchinja kafara na ‘ibaadah zangu na uhai wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Allaah Pekee Rabb wa walimwengu. Hana mshirika, na kwa hayo ndio nimeamrisha, nami ni Muislamu wa kwanza)) [29]

وَمِنَ السُّنَّةِ: ((لَعَنَ اللَّهُ مَنْ ذَبَحَ لِغَيْرِ اللَّهِ))

Na katika Sunnah: ((Allaah Amemlaani aliyechinja kwa ajili ya asiye kuwa Allaah)).[30]

Na dalili ya An-Nadhr (nadhiri) kauli Yake Ta'aalaa:

يُوفُونَ بِالنَّذْرِ وَيَخَافُونَ يَوْمًا كَانَ شَرُّهُ مُسْتَطِيرًا (٧)

((Ambao) Wanatimiza nadhiri na wanaiogopa siku ambayo shari yake ni yenye kuenea kwa upana))[31]

Msingi Wa Pili: Kuijua Dini Ya Kiislamu Kwa Dalili

Nayo ni kujisalimisha kwa Allaah kwa Tawhiyd, na kunyenyekea katika utiifu, na kujiweka mbali na shirki pamoja na watu wake (wa

shirki), nao (huo Msingi wa pili) umegawanyika katika daraja tatu; Uislamu, Iymaan, Ihsaan. Na kila daraja ina nguzo.

Daraja Ya Kwanza: Uislamu

فَأَرْكَانُ الْإِسْلَامِ خَمْسَةٌ:

((شَهَادَةُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ، وَإِقَامُ الصَّلَاةِ، وَإِيتَاءُ الزَّكَاةِ، وَصَوْمُ رَمَضَانَ، وَحَجُّ بَيْتِ اللَّهِ الْحَرَامِ))

Na nguzo za Kiislamu ni tano:

((Kushuhudia kwa kukiri kwa moyo na kutamka kwamba laa ilaaha illa-Allaah - hakuna Muabudiwa wa haki isipokuwa Allaah, na kwamba Muhammad ni Rasuli wa Allaah, na kusimamisha Swalaah, na kutoa Zakaah, na kufunga Swawm Ramadhwaan, na kuhiji Nyumba Tukufu ya Allaah))[32]

Na dalili ya Shahada ni kauli Yake Ta'aalaa:

شَهِدَ اللَّهُ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ وَالْمَلَائِكَةُ وَأُولُو الْعِلْمِ قَائِمًا بِالْقِسْطِ
لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ (١٨)

((Allaah Ameshuhudia kwamba hapana Muabudiwa wa haki ila Yeye; na Malaika, na wenye elimu (wameshuhudia kwamba Allaah) ni Mwenye kusimamisha (uumbaji Wake) kwa uadilifu. Hapana Muabudiwa wa haki ila Yeye Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika, Mwenye hikmah wa yote))[33]

Na maana yake ni: Hakuna Muabudiwa wa haki ila Allaah Pekee. ((**Laa ilaaha – hakuna muabudiwa wa haki**)) inakanusha kila kinachoabudiwa pasi na Allaah. Ama ((**illa-Allaah – isipokuwa Allaah**)) inathibitisha 'ibaadah zote ni kwa ajili ya

Allaah Pekee. Hana mshirika katika ‘ibaadah Zake kama Alivyokuwa hana mshirika katika Ufalme Wake.

Na tafsiri inayobainisha wazi (Shahaadah), ni kauli Yake Ta’aalaa:

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ إِنَّنِي بَرَاءٌ مِّمَّا تَعْبُدُونَ (٢٦) إِلَّا الَّذِي فَطَرَنِي فَإِنَّهُ سَيَهْدِينِ (٢٧) وَجَعَلَهَا كَلِمَةً بَاقِيَةً فِي عَقِبِهِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ (٢٨)

((Na Ibraahiym alipomwambia baba yake na kaumu yake: “Hakika mimi nimejitoa katika dhima na yale mnayoyaabudu. “Isipokuwa Ambaye Ameniumba, basi hakika Yeye Ataniongoza.” Na akalifanya neno (la ilaaha illaa-Allaah) lenye kubakia katika kizazi chake ili wapate kurejea.))[34]

Na kauli Yake Ta’aalaa:

قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْا إِلَىٰ كَلِمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَّا نَعْبُدَ إِلَّا اللَّهَ وَلَا نُشْرِكَ بِهِ شَيْئًا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّهِ فَإِن تَوَلَّوْا فَقُولُوا اشْهَدُوا بِأَنَّا مُسْلِمُونَ (٦٤)

((Sema: “*Enyi Ahlal-Kitaabi!* Njooni katika neno lililo sawa baina yetu na baina yenu, kwamba tusiabudu isipokuwa Allaah Pekee, na wala tusimshirikishe na chochote, na wala wasichukue baadhi yetu wengine kuwa waungu badala ya Allaah.” Wakikengeuka; basi semeni: “Shuhudieni kwamba sisi ni Waislaam tunajisalimisha kwa Allaah.”))[35]

Na dalili ya kushuhudia kwamba Muhammad ni Rasuli wa Allaah ni kauli Yake Ta’aalaa:

لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُمْ
بِالْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ (١٢٨)

((Kwa yakini amekujieni Rasuli anayetokana na nyinyi wenyewe, yanamtia mashaka (na huzuni) yanayokutaabisheni, anakujalini (muongoke) mwenye huruma kwa Waumini ni mwenye huruma mno, mwenye rahmah))[36]

Na maana ya kushuhudia kwamba Muhammad ni Rasuli wa Allaah, ni kumtii yale aliyoyaamrisha, na kumsadikisha katika aliyoyajulisha, na kujiepusha na ambayo ameyakataza na aliyoyatahadharisha, na kwamba Allaah asiabudiwe isipokuwa kwa kufuata yale yaliyowekewa Shariy'ah.

Na dalili ya Swalaah na Zakaah na tafsiri ya At-Tawhiyd ni kauli Yake Ta'aalaa:

وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ حُنَفَاءَ وَيُقِيمُوا
الصَّلَاةَ وَيُؤْتُوا الزَّكَاةَ وَذَلِكَ دِينُ الْقَيِّمَةِ (٥)

((Na hawakuamrisha isipokuwa wamwabudu Allaah wenye kumtakasia Dini, wenye kujiengua na upotofu kuelemea Dini ya haki na wasimamishe Swalaah na watoe Zakaah; na hiyo ndiyo Dini iliyosimama imara.))[37]

Na dalili ya Swiyaam ni kauli Yake Ta'aalaa:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِن
قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ (١٨٣)

((Enyi walioamini! Mmeandikiwa shariy'ah ya kufunga Swiyaam kama ilivyoandikwa kwa walio kabla yenu mpate kuwa na taqwa.))
[38]

Na dalili ya Hajj ni kauli Yake Ta'aalaa:

وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا وَمَنْ كَفَرَ
فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ (٩٧)

((Na kwa ajili ya Allaah ni wajibu kwa watu watekeleze Hajj katika Nyumba hiyo kwa mwenye uwezo. Na atakayekufuru, basi hakika Allaah ni Mkwasi kwa walimwengu.))[39]

Daraja Ya Pili: Iymaan

وَهُوَ:

((بَضْعٌ وَسَبْعُونَ شُعْبَةً، فَأَعْلَاهَا قَوْلُ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَأَدْنَاهَا
إِمَاطَةُ الْأَذَى عَنِ الطَّرِيقِ، وَالْحَيَاءُ شُعْبَةٌ مِنَ الْإِيمَانِ))

Nayo ni:

((Ina tanzu [matawi] sabiini na kitu. Ya juu yake ni kauli ya “laa ilaaha illa-Allaah” [hapana Muabudiwa wa haki ila Allaah], na ya chini yake kabisa ni kuondosha uchafu njiani. Na kuona hayaa ni utanzu [tawi] katika tanzu za imani))[40]

وَأَرْكَانُهُ سِتَّةٌ كَمَا فِي الْحَدِيثِ:

((أَنْ تُؤْمِنَ بِاللَّهِ، وَمَلَائِكَتِهِ، وَكُتُبِهِ، وَرُسُلِهِ، وَالْيَوْمِ الْآخِرِ،
وَتُؤْمِنَ بِالْقَدَرِ خَيْرِهِ وَشَرِّهِ))

Na nguzo zake ni sita kama katika Hadiyih:

((Ni kumwamini Allaah, na Malaika Wake, na Vitabu Vyake, na Rasuli Wake na Siku ya Mwisho, na kuamini Al-Qadr [majaaliwa] ya kheri na shari zake)).[41]

Na dalili ya hizi nguzo sita ni kauli Yake Ta'aalaa:

لَيْسَ الْبِرَّ أَنْ تُوَلُّوا وُجُوهَكُمْ قِبَلَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَلَكِنَّ الْبِرَّ
مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالْكِتَابِ وَالنَّبِيِّينَ

((Si wema (pekee) kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa Mashariki na Magharibi lakini wema (khaswa) ni mwenye kuamini Allaah na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii))[42]

Na dalili ya Al-Qadr (majaaliwa) ni kauli ya Allaah:

إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ (٤٩)

((Hakika sisi Tumekiumba kila kitu kwa makadirio))[43]

Daraja Ya Tatu: Ihsaan

رُكْنٌ وَاحِدٌ كَمَا فِي الْحَدِيثِ: ((أَنْ تَعْبُدَ اللَّهَ كَأَنَّكَ تَرَاهُ، فَإِنْ لَمْ تَكُنْ
تَرَاهُ فَإِنَّهُ يَرَاكَ))

Nguzo yake ni moja kama katika Hadiyth: ((Umwabudu Allaah kama kwamba unamuona, na hata kama humuoni, basi Yeye Anakuona))[44]

Na dalili ni kauli Yake Ta'aalaa:

إِنَّ اللَّهَ مَعَ الَّذِينَ اتَّقَوْا وَالَّذِينَ هُمْ مُحْسِنُونَ (١٢٨)

((Hakika Allaah Yu Pamoja na wenye taqwa, na wale ambao wao ni wenye kufanya ihsaan.))[45]

Na kauli Yake Ta'aalaa:

وَتَوَكَّلْ عَلَى الْعَزِيزِ الرَّحِيمِ (٢١٧) الَّذِي يَرَاكَ حِينَ تَقُومُ (٢١٨)
وَتَقْلُبَكَ فِي السَّاجِدِينَ (٢١٩) إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ (٢٢٠)

((Na tawakali kwa Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika, Mwenye kurehemu. Ambaye Anakuona wakati unaposimama. Na mageuko yako katika wenye kusujudu. Hakika Yeye Ndiye Mwenye kusikia yote, Mjuzi wa yote))[46]

Na kauli Yake Ta'aalaa:

وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُو مِنْهُ مِنْ قُرْآنٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ
إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ ۚ

((Na hushughuliki katika jambo lolote, na wala husomi humo katika Qur-aan, na wala hamtendi 'amali yoyote isipokuwa Tunakuwa Mashahidi juu yenu mnaposhughulika nayo))[47].

Na dalili katika Sunnah ni Hadiyth mashuhuri ya Jibriyl:

عَنْ عُمَرَ بْنِ الْخَطَّابِ (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) قَالَ: بَيْنَمَا نَحْنُ جُلُوسٌ
عِنْدَ النَّبِيِّ (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) إِذْ طَلَعَ عَلَيْنَا رَجُلٌ، شَدِيدُ
بَيَاضِ الثِّيَابِ، شَدِيدُ سَوَادِ الشَّعْرِ، لَا يُرَى عَلَيْهِ أَثَرُ السَّفَرِ، وَلَا
يَعْرِفُهُ مِنَّا أَحَدٌ، فَجَلَسَ إِلَى النَّبِيِّ (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ)
فَأَسْنَدَ رُكْبَتَيْهِ إِلَى رُكْبَتَيْهِ، وَوَضَعَ كَفَّيْهِ عَلَى فَخْذَيْهِ، وَقَالَ: يَا
مُحَمَّدُ أَخْبِرْنِي عَنِ الْإِسْلَامِ فَقَالَ: ((أَنْ تَشْهَدَ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ
مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ، وَتُقِيمَ الصَّلَاةَ، وَتُؤْتِيَ الزَّكَاةَ، وَتَصُومَ
رَمَضَانَ، وَتَحُجَّ الْبَيْتَ إِنْ اسْتَطَعْتَ إِلَيْهِ سَبِيلًا)) قَالَ: صَدَقْتَ.
فَعَجَبْنَا لَهُ يَسْأَلُهُ وَيُصَدِّقُهُ. قَالَ: أَخْبِرْنِي عَنِ الْإِيمَانِ. قَالَ: ((أَنْ
تُؤْمِنَ بِاللَّهِ، وَمَلَائِكَتِهِ، وَكُتُبِهِ، وَرُسُلِهِ، وَالْيَوْمِ الْآخِرِ، وَتُؤْمِنَ

بِالْقَدْرِ خَيْرِهِ وَشَرِّهِ)) قَالَ: صَدَقْتَ. قَالَ: أَخْبِرْنِي عَنِ الْإِحْسَانِ. قَالَ: ((أَنْ تَعْبُدَ اللَّهَ كَأَنَّكَ تَرَاهُ، فَإِنْ لَمْ تَكُنْ تَرَاهُ فَإِنَّهُ يَرَاكَ)) قَالَ: أَخْبِرْنِي عَنِ السَّاعَةِ. قَالَ: ((مَا الْمَسْئُولُ عَنْهَا بِأَعْلَمَ مِنَ السَّائِلِ)) قَالَ: فَأَخْبِرْنِي عَنْ أَمَارَاتِهَا. قَالَ: ((أَنْ تَلِدَ الْأُمَةُ رَبَّتَهَا، وَأَنْ تَرَى الْحَفَاةَ الْعُرَاةَ الْعَالَةَ رِعَاءَ الشَّيْءِ يَتَطَاوَلُونَ فِي الْبُنْيَانِ)) قَالَ: فَمَضَى، فَلَبِثْنَا مَلِيًّا، فَقَالَ: ((يَا عُمَرُ أَتَدْرُونَ مَنْ السَّائِلُ؟)) قُلْنَا: اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَعْلَمُ، قَالَ: ((هَذَا جِبْرِيلُ أَتَاكُمْ يُعَلِّمُكُمْ أَمْرَ دِينِكُمْ)).

Imepokelewa kutoka kwa 'Umar (رضي الله عنه) amesema: Siku moja tulikuwa tumekaa na Nabiyy (صلى الله عليه وآله وسلم), hapo alitokea mtu ambaye nguo zake zilikuwa nyeupe pepe na nywele zake zilikuwa nyeusi sana; hakuwa na alama ya machofu ya safari na wala hapakuwa na hata mmoja katika sisi aliyemtambua. Alienda akakaa karibu na Nabiyy (صلى الله عليه وآله وسلم) akaweka magoti yake karibu na magoti yake na akaweka viganja vyake juu ya mapaja yake, kisha akasema; Ee Muhammad! Niambie kuhusu Uislamu. Akasema: ((Ni kushuhudia kwa kukiri na kwa moyo kuwa hakuna Muabudiwa wa haki isipokuwa Allaah, na Muhammad ni Rasuli Wake, kusimamisha Swalaah, kutoa Zakaah, kufunga Swawm Ramadhwaan na kwenda kuhiji [Makkah] ukiweza)) Akasema yule mtu yaani Jibriyl: Umesema kweli. Tulipigwa na mshangao kwa kumuuliza kwake na kumsadikisha. Na akasema tena: Niambie kuhusu Iymaan. Akasema: ((Ni kumwamini Allaah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Rasuli Wake na Siku ya Mwisho, na kuamini Al-Qadr kheri na shari zake)) Akasema: Umesema kweli. Akasema: Hebu nielezee kuhusu Ihsaan. Akasema: ((Ni kumuabudu Allaah kama vile unamuona na hata kama humuoni basi Yeye Anakuona)). Akasema: Niambie kuhusu Qiyaamah. Akajibu: ((Muulizwaji si mjuzi kama asivyo vilevile muulizaji)) Kisha akamwambia: Nijulishe alama zake: Akajibu: ((Kijakazi atazaa bibi yake, na utaona wachunga wenda miguu chini, wenda uchi [wasio na uwezo wa kumiliki hata mavazi], mafukara [wasiokuwa hata na sehemu ya kuishi kwa umaskini] wakishindana kujenga majumba ya fahari.)).

Kisha [Jibriyl] akaondoka na nilitulia kidogo [nikitafakari]. Kisha Nabiyy (صلى الله عليه وآله وسلم) akasema: ((Ee 'Umar! Je, mnamjua ni nani yule aliyekuwa akiuliza?)) Nikasema: Allaah na Rasuli Wake wanajua zaidi. Akasema: ((Ni Jibriyl, alikuja kuwafundisha Dini yenu)) [48]

Msingi Wa Tatu: Kumjua Nabiyy Wenu Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم)

Naye ni Muhammad bin ‘Abdillaah bin ‘Abdil-Muttwalib bin Haashim. Na Haashim ni kutoka katika (kabila la) la Quraysh. Na Quraysh ni katika Waarabu. Na Waarabu ni kutokana na kizazi cha Ismaa’iyl bin Ibraahiym Al-Khaliyl Swalaah na salamu bora kabisa ziwafikie yeye na Nabiyy wetu. Naye alikuwa na umri wa miaka sitini na tatu, miongoni mwa miaka hiyo miaka arubaini kabla ya kupewa Unabiyy, na miaka ishirini na tatu akiwa katika Unabiyy. Akapewa Unabiyy kwa: **((Iqraa - Soma))** na akatumwa (kulingania) kwa **((Al-Muddath-thir – mwenye kujigubika))**. Na nchi yake ni Makkah. Allaah Amemtuma kuonya kuhusu shirki na kulingania katika Tawhiyd.

Na dalili ni kauli Yake Ta’aalaa:

يَا أَيُّهَا الْمُدَّثِّرُ (١) قُمْ فَأَنذِرْ (٢) وَرَبَّكَ فَكَبِّرْ (٣) وَثِيَابَكَ فَطَهِّرْ
(٤) وَالرُّجْزَ فَاهْجُرْ (٥) وَلَا تَمْنُنْ تَسْتَكْثِرُ (٦) وَلِرَبِّكَ فَاصْبِرْ
(٧)

((Ee mwenye kujigubika! Simama na uonye. Na Rabb wako mtukuze. Na nguo zako toharisha. Na najisi (masanamu) epukana nayo. Na wala usifanye fadhila kwa ajili ya kutaraji kukithirishiwa. Na kwa ajili ya Rabb wako subiri)) [49]

Amesimamia haya miaka kumi akilingania katika Tawhiyd. Na baada ya miaka kumi, alipandishwa mbinguni (Mi’iraaaj) na

akafaridhishwa Swalaah tano, akaswali Makkah miaka mitatu, na baada ya hapo akaamrishwa kuhajiri kwenda Madiynah. Na hijrah ni kuhama kutoka nchi ya shirki kwenda katika nchi ya Kiislamu.

Na hijrah ni fardhi kwa Ummah huu kuhama kutoka katika nchi ya shirki kwenda nchi ya Kiislamu. Nayo itaendelea kubakia hadi itakaposimama Saa (Qiyaamah).

Na dalili ni kauli Yake Ta'aalaa:

إِنَّ الَّذِينَ تَوَفَّاهُمُ الْمَلَائِكَةُ ظَالِمِي أَنْفُسِهِمْ قَالُوا فِيمَ كُنْتُمْ ۖ قَالُوا كُنَّا مُسْتَضْعَفِينَ فِي الْأَرْضِ ۗ قَالُوا أَلَمْ تَكُنْ أَرْضُ اللَّهِ وَاسِعَةً ۖ فَتُهَاجِرُوا فِيهَا ۗ فَأُولَئِكَ مَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ ۖ وَسَاءَتْ مَصِيرًا (٩٧) إِلَّا الْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَاءِ وَالْوِلْدَانِ لَا يَسْتَطِيعُونَ حِيلَةً وَلَا يَهْتَدُونَ سَبِيلًا (٩٨) فَأُولَئِكَ عَسَى اللَّهُ أَنْ يَغْفُو عَنْهُمْ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَفُورًا غَفُورًا (٩٩)

((Hakika wale ambao Malaika wamewafisha, hali wamejidhulumu nafsi zao; (Malaika) watawaambia: “Mlikuwa katika hali gani?” Watasema: “Tulikuwa tukikandamizwa katika ardhi.” (Malaika) Watasema: “Je, kwani ardhi ya Allaah haikuwa ya wasaa mkahajiri? Basi hao makazi yao yatakuwa ni Jahannam, na uovu ulioje mahali pa kuishia. Isipokuwa wale waliokandamizwa kati ya wanaume na wanawake na watoto ambao hawakuweza kupata (mpango wa) hila yoyote wala hawawezi kuongoza njia. Basi hao asaa Allaah Akawasamehe. Na Allaah daima ni Mwingi wa kusamehe, Mwingi wa kughufuria))[50]

Na kauli Yake Ta'aalaa:

يَا عِبَادِيَ الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّ أَرْضِي وَاسِعَةً فَإِيَّايَ فَاعْبُدُونِ (٥٦)

((“Enyi waja Wangu walioamini! Hakika ardhi Yangu ni pana, basi Mimi Pekee Niabuduni.”))[51]

Amesema Al-Baghaawiy (رحمه الله): “Aayah hii imeteremshwa kwa sababu ya Waislamu waliokuwa Makkah ambao hawakuhajiri. Allaah Amewaita kwa jina la Waumini.

Na dalili ya Hijrah (kuhajiri) katika Sunnah ni kauli yake (صلى الله عليه وآله وسلم):

((Hijrah haikatiki mpaka ikatike tawbah. Na tawbah haikatiki mpaka jua lichomoze kutoka Magharibi))[52]

Baada ya kustakiri Madiynah aliamrisha Shariy’ah za Kiislamu zilobakia kama; Zakaah, Swawm, Hajj, Adhaan, Jihaad, kuamrisha mema na kukataza munkari na mengineyo ya Shariy’ah ya Kiislamu. Amefanya hayo miaka kumi akafariki baada ya hapo, Swalaah na salamu ziwe juu yake. Na Dini yake imebaki. Na hii Dini yake, hakuna kheri isipokuwa kawaelekeza kwayo Ummah, na hakuna shari ila amewatahadharisha nayo. Na kheri aliyowaongoza kwayo ni Tawhiyd na yote Anayoyapenda Allaah na Anayoyaridhia. Na shari ambazo amezitahadharisha ni shirki na yote yanayomchukiza Allaah na Asiyoyaridhia. Allaah Amemtuma kwa watu wote, na Amefaradhisha *Ath-Thaqalayn* (walimwengu wawili); majini na watu kumtii yeye (Nabiy).

Na dalili ni kauli Yake Ta’aalaa:

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا

((Sema (ee Muhammad صلى الله عليه وآله وسلم): “Hakika mimi ni Rasuli wa Allaah kwenu nyinyi nyote.))[53]

Na Allaah Ameikamilisha Dini hii kwa kupitia kwake. Na dalili ni kauli ya Yake Ta’aalaa:

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتِمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا

((Leo Nimekukamilishieni Dini yenu, na Nimekutimizieni neema Yangu, na Nimekuridhieni Uislaam uwe Dini yenu.))[54]

Na dalili ya kifo chake (صلى الله عليه وآله وسلم) ni kauli Yake Ta'aalaa:

إِنَّكَ مَيِّتٌ وَإِنَّهُمْ مَيِّتُونَ (٣٠) ثُمَّ إِنَّكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عِنْدَ رَبِّكُمْ تَخْتَصِمُونَ (٣١)

((Hakika wewe (ee Muhammad صلى الله عليه وآله وسلم) utakufa nao pia watakufa. Kisha hakika nyinyi Siku ya Qiyaamah mtakhasimiana mbele ya Rabb wenu.))[55]

Na watu watakapokufa watafufuliwa.

Na dalili ni kauli Yake Ta'aalaa:

مِنْهَا خَلَقْنَاكُمْ وَفِيهَا نُعِيدُكُمْ وَمِنْهَا نُخْرِجُكُمْ تَارَةً أُخْرَىٰ (٥٥)

((Kutokana nayo (ardhi) Tumekuumbeni, na humo Tutakurudisheni, na kutoka humo Tutakutoeni mara nyingine))[56]

Na kauli Yake Ta'aalaa:

وَاللَّهُ أَنْبَتَكُمْ مِّنَ الْأَرْضِ نَبَاتًا (١٧) ثُمَّ يُعِيدُكُمْ فِيهَا وَيُخْرِجُكُمْ إِخْرَاجًا (١٨)

((Na Allaah Amekuanzisheni vizuri katika (udongo wa) ardhi. Kisha Atakurudisheni humo na Atakutoeni tena mtoke (kuwa hai)) [57]

.Na baada ya kufufuliwa watahesabiwa na watalipwa kwa 'amali zao

Na dalil ni kauli Yake Ta'aalaa:

وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ لِيَجْزِيَ الَّذِينَ أَسَاءُوا بِمَا
عَمِلُوا وَيَجْزِيَ الَّذِينَ أَحْسَنُوا بِالْحُسْنَى (٣١)

((Na ni vya Allaah Pekee vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini ili Awalipe wale waliofanya uovu kwa yale waliyoyatenda, na Awalipe wale waliofanya mema kwa mema zaidi))[58]

Na anayekadhibisha kufufuliwa amekufuru.

Na dalili ni kauli Yake Ta'aalaa:

زَعَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنْ لَّنْ يُبْعَثُوا قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتُبْعَثَنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤَنَّ
بِمَا عَمِلْتُمْ ۚ وَذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ (٧)

((Waliokufuru wamedai kwamba hawatofufuliwa kamwe. Sema: Bali hapana! Naapa kwa Rabb wangu, bila shaka mtafufuliwa, kisha mtajulishwa kwa yale mliyoyatenda, na hayo kwa Allaah ni mepesi.))[59]

Na Allaah Ametuma Rasuli wote wakiwa ni wabashiriaji na waonyaji.

Na dalili ni kauli Yake Ta'aalaa:

رُسُلًا مَّبَشِّرِينَ وَمُنْذِرِينَ لِّنَّا لِيَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ
الرُّسُلِ ۚ

((Rasuli ni wabashiriajina waonyaji ili pasikuweko kutoka kwa watu hoja yoyote juu ya Allaah baada ya (kuletwa) Rasuli))[60]

Na wa kwanza wao ni Nuwh (عليه السلام) na wa mwisho wao ni Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم) naye ndiye Nabiy wa mwisho.

Na dalili kwamba Nuuh ndio wa mwanzo wao ni kauli Yake Ta'aalaa:

إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَى نُوحٍ وَالنَّبِيِّينَ مِنْ بَعْدِهِ ۚ

((Hakika Tumekufunulia Wahy (ee Muhammad صلى الله عليه وآله وسلم) kama Tulivyomfunulia Wahy Nuwh na Nabiy baada yake))[61]

Na kila Ummah Allaah Ameupelekea Rasuli kuanzia Nuwh hadi kwa Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم). Akiwaamrisha kumwabudu Allaah Pekee, na Akiwakataza kuabudu twaghuti[62]

Na dalili ni kauli Yake Ta'aalaa:

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنْ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ ۚ

((Na kwa yakini Tulituma katika kila ummah Rasuli (alinganie) kwamba: “Mwabuduni Allaah na jiepusheni na taghuti))[63].

Na Allaah Akafaridhisha kwa waja wote wakanushe twaghuti na kumwamini Allaah (wamwabudu Yeye Pekee).

Ibnul Qayyim (رحمه الله) amesema: “Maana ya twaghuti ni kila anachopindukia mja mipaka yake; ikiwa ni kinachoabudiwa, au kinachofuatwa au kinachotiiwa. Na matwaghuti ni wengi. Wakuu wao ni watano; Ibliys laana za Allaah ziwe juu yake, na anayeabudiwa hali ya kuwa yeye yuko radhi, na anayeita watu wamwabudu yeye, na anayedai kujua elimu ya ghayb (isiyoonekana na kujulikana isipokuwa na Allaah), na anayehukumu yale ambayo Hakuyateremsha Allaah.”

Na dalili ni kauli Yake Ta'aalaa:

لَا إِكْرَاهَ فِي الدِّينِ ۚ قَدْ تَبَيَّنَ الرُّشْدُ مِنَ الْغَيِّ ۚ فَمَنْ يَكْفُرْ بِالطَّاغُوتِ
وَيُؤْمِن بِاللَّهِ فَقَدْ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ لَا انْفِصَامَ لَهَا ۗ وَاللَّهُ
سَمِيعٌ عَلِيمٌ (٢٥٦)

((Hapana kulazimisha katika (kuingia) Dini, kwani imekwishabainika kati ya uongofu na upotofu. Basi atakayemkanusha twaaghuwt (miungu ya uongo) na akamwamini Allaah kwa hakika atakuwa ameshikilia imara kishikilio madhubuti kisichovunjika, na Allaah ni Mwenye kusikia yote, Mjuzi wa yote)) [64]

Na hii ndio maana ya *Laa ilaaha illa-Allaah* (hapana Muabudiwa wa haki isipokuwa Allaah).

وَفِي الْحَدِيثِ: ((رَأْسُ الْأَمْرِ الْإِسْلَامُ، وَعَمُودُهُ الصَّلَاةُ، وَذِرْوَةٌ
سَنَامِهِ الْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ))

Na katika Hadiyith: ((Msingi wa mambo ni Uislamu, na nguzo yake ni Swalaah na kilele cha nundu yake ni kupigana katika njia ya Allaah))/65/